

REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THE HANSARD

Tuesday, 3rd July, 2018

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 2.30 p.m.*

[The Temporary Speaker (Hon. Thaura) in the Chair]

PRAYERS

MOTION

ADOPTION OF THE REPORT ON THE STATUS OF COUNTY PLOUGHING TRACTORS

THAT, this House adopts the Report of the Agriculture, Livestock and Fisheries Committee on the status of County ploughing tractors laid on the Table of this House on 8th May, 2018.

(Hon. (Ms.) Messo on 13.6.2018)

(Resumption of Debate interrupted on 13.6.2018)

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Hon. Members, this Motion was moved on the 13th June, 2018, by hon. (Ms.) Messo and seconded by hon. Christopher Mwambire who represents Bamba Ward. So today we resume our contributions towards the Motion. The Floor is now open for debate. I believe those who were in the Committee can start for us please. Yes hon. Mwanganda Gogo.

Hon. Gogo: Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii ili kuchangia machache juu ya swala hili ambalo lilikuja Bungeni mwezi wa pili mwaka huu na mheshimiwa Kenga. Nilikuwa nikitupa macho nione kama mheshimiwa yuko ili nimjibu lakini simuoni. Wacha niendeleo kwa kusema kwamba tarehe 12 mwezi wa pili, mheshimiwa alileta ombi kwa Waziri wa Kilimo kupitia Kamati ya Kilimo na aliulizwa ikiwa Waziri wa kitengo hicho anajua ya kwamba *tractors* nyingi ndani ya Kilifi Kaunti hazifanyi kazi.

Mimi nikiwa mmoja wa wanakamati tulibeba hilo swala kwa uzito hasa tukijua kilimo ndio uti wa mgongo kwa sisi watu wa Kilifi. Tulizunguka na wakati akitoa ombi hilo kulikuwa na *tractors* kumi ambazo zilikuwa hazifanyi kazi tukiwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa wa Kaloleni na hivi tunavyozungumza hizo *tractors* ziko tayari zinafanya kazi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kile ningeomba wabunge wenzangu ni msamaha kwa sababu hata kama *tractors* nyingi zinafanya kazi lakini tumechelewa kwa sababu wakati huu kilimo kinafaa kianze mwezi wa tatu au wa nne lakini umefika mwezi wa saba sasa na ziko tayari.

Kwa niaba ya Kamati na waheshimiwa wenzangu na watu wa Kilifi tunaomba Bunge letu hili, kusema poleni lakini imani yetu ni kwamba Mungu akituweka hai tukiingia mwaka ujao, *tractors* zote zitakuwa tayari na kilimo kitaanza mapema sana. Kwa sasa tumejaribu kama Kamati na karibu zote zinafanya kazi. Naomba wabunge wenzetu mtukubali na huu Msawaada muupitisha ili kazi iendelee. Asante sana.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Yes hon. Mramba.

Hon. Mramba: Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi nami napenda kuchangia Hoja iliyo mbele yetu. Kwanza Ripoti ilipoletwa haingeweza kujadiliwa siku ya kwanza kwa sababu Mheshimiwa Kenga alikuwa ndiye anakalia kiti cha Spika hivyo basi ikasemekana hakuwa na fursa ya kuweza kutetea ama kuchangia Ripoti hii. Ukweli ni kwamba *tractors* zimenunuliwa kwa pesa nyingi lakini hazifanyi kazi. Huo ndio ukweli na lazima tuukubali.

Idara inayosimamia zile *tractors* haifanyi kazi kama inavyotarajiwa na wananchi. Nikitoa mfano mmoja, zile *tractors* ambazo zinasemekana zimelala ni mpya lakini zilikuwa hazijasajiliwa. Kwanza tunataka kujua na je Kamati ilitaka kujua ni kwa nini *tractors* zimekaa mwaka mzima bila kusajiliwa? Na yule aliyesababisha zile *tractors* zisisajiliwe ni nani na ni kwa nini? Tunatakikana maswala kama haya tuweze kujibiwa kwanza kabla hatujaenda mbele.

Mheshimiwa Spika, unapoenda kufanya mtihani wa kidato cha nne na uanguke mtihani, ukiamua kurudia ni sharti ujue na kitu gani kilikufanya uanguke mara ya kwanza, bila hivyo utaanguka tena. Wale wale waliosababisha *tractors* hizi zikae bila kusajiliwa kwa mwaka mzima wako pale pale kazini mpaka leo. Tunahitaji kujua ni akina nani na walifanya hivyo na kwa nini. Ninavyokwambia Mheshimiwa na wabunge wenzangu ni kwamba utaona *tractors* ziko hapa ya Jilore, Kakuyuni na ya Malindi. *Tractor* ikitoka hapa mpaka Madunguni ambako ndio inalima...

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Is it a Point Of Order mheshimiwa? Yes hon. Christopher Mwambire.

Hon. Mwambire: Asante mheshimiwa Spika. Nimesimama kupinga kuendelea kwa hotuba ambayo Mheshimiwa wa Kakuyuni anaendelea kuelezea ikiwa mimi ni mwanakamati wa Kamati ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi. Mheshimiwa Mramba labda hajapata nakala ya Ripoti ya ukaguzi wa Kamati iliyofanya kuhusu Hoja ambayo tunaijadili ya kutafuta na kuona kwamba *tractors* hazifanyi kazi kwa nini? Mjadala ambao uliletwa mbele ya Nyumba hii na Mheshimiwa Kenga. Ningependa kuelza kupitia kwako Bw. Spika ili aweze kupata ufahamu zaidi kama Mwanakamati katika Kamati hii ya Kilimo.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): I think hon. Mramba is right to ask whether it is Information or Point of Order.

Hon. Mwambire: Point Of Information.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Then you should have consulted him whether he would like to be informed before you make your submission. Okay, Hon. Mramba, do wish to be informed?

Hon. Mramba: Bw Spika, sihitaji kufahamishwa kwa sababu ninayo fahamu na ninaelewa kile ninachosema. Nimetangulia kusema wale waliotutatiza wako pale serikalini na ni lazima tuwajue ni akina nani na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao bila hivyo tutakuwa hatufanyi lolote. Nikiendelea hivyo ni kwamba *tractor* itatoka Malindi hapa iende Madunguni,

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ikifika Madunguni itakaa siku tatu kwa sababu haina mafuta. Ikianza kulima, dereva anakuja saa tatu analima ikifika saa tisa dereva anafunga kazi...

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Hon. Mwanganda what is your Point of Order please?

Hon. Mwanganda: Asante Mheshimiwa Spika. Nitaanzia pale mheshimiwa mwenzangu alipokuwa ameachia lakini yangu ni *Point of Order*; nafikiri swali ambalo mheshimiwa Stanley Kenga ameuliza hapa Bungeni alikuwa anauliza “Je waziri anajua ni kwa nini matingatinga mengi ya Kaunti ya Kilifi hayafanyi kazi?” Haikuwa ni swali juu ya *tractors* kumi ambazo zilikuwa hazina nambari za usajili. Ndiposa Kamati hii ilichukua hilo swala la kutafuta ni kwa nini zile *tractors* zote za Kaunti ya Kilifi hazifanyi kazi. Kwa hivyo, mheshimiwa wa Kakuyuni akisema kwamba ilikuwa ni tuangalie ni kwa nini hizo *tractors* 10 zilikuwa hazijasajiliwa sababu yake ni nini ndio tulete Ripoti Bungeni, atakuwa anaenda nje ya hii mada.

Swali lilikuwa ni “Je kama Kamati na waziri wa Kilimo anajua ni kwa nini matingatinga mengi ndani ya Kaunti ya Kilifi hayafanyi kazi?” Nafikiri ni Ripoti ambayo tumepeana na Kamati yetu imeeleza kila kitu ni kwa nini hayo matingatinga hayafanyi kazi. Asante sana.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Okay, thank you. Wind up your time is almost up hon. Mramba.

Hon. Mramba: Mheshimiwa Spika, mimi sidhani nimeenda nje ya Mada na ninachosema ni kwamba mheshimiwa Stanley Kenga hakueleza ni *tractors* ngapi ambazo zimelala. Aliuliza ni kwa nini *tractors* nyingi zimelala na kati ya zile zilizolala kuna *tractors* kumi zilikuwa ni mpya lakini hazijapata kusajiliwa. Kosa langu ni nini? Ninachouliza ni kwamba zingine zilikuwa zimelala na kuna zingine ni mpya zimekuja hazijasajiliwa; ni kwa nini hazikusajiliwa mapema zikafanya kazi?

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Yes, your parting shot mheshimiwa?

Hon. Mramba: Kwa hivyo, mimi ninachoomba ni kwamba hapa kwenye Ripoti hakujaelezwa yule aliyesababisha mpaka *tractors* zile zisisajiliwe na ni hatua gani ambayo imependekezwa kwa mtu huyo. Ninachoomba ni kwamba Kamati hii irudi tena itwambie waliosababisha mpaka *tractors* hazikusajiliwa ni akina nani na ni kwa nini? Asante sana mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Hon. (Ms.) Elina Mbaru.

Hon. (Ms.) Elina: Asante sana mheshimiwa Spika. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kamati inavyoeleza nataka kupingana nayo kabisa. Hivi ninavyozungumza *tractor* ya Magarini iko marekebuni na imelala. Iko kwa familia ya kwa mzee Kuto imewekwa tangu mwezi wa tano mpaka sasa kwa sababu ilipasuka *filter* ya mafuta. Wakisema trekta zote zinafanya kazi ninakanusha kabisa kama Kamati. Na kama wanataka ushahidi, naomba nitoke nao leo, sio kesho, twende sote wakaone trekta ambayo imelala pale. Kwa hivyo, ningetaka kusema kwamba hii Kamati haijafanya utendakazi kikamilifu, waende tena wakae kama vile mheshimiwa Mramba alivyozungumza...

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Someone wants to inform you.

Hon. (Ms.) Elina: No! no! no!

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Okay she does not need your information.

Hon. (Ms.) Elina: Yeye ni Mwanakamati katika ile Kamati tunataka kumuongezea kazi aanze upya kwa hivyo tunavyozungumza matrekta bado hata mengine bado hayaja...

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Yes, what is your Point of Order?

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.

Hon. Noordin: Asante sana mheshimiwa Spika. Nimesimama kwa Hoja ya nidhamu. Nataka kumkosoa mheshimiwa Elina Mbaru, kwamba kuna tofauti ya vitu ambavyo vinatengenezwa kuendelea kufanya kazi na mijengo. Vitu ambavyo tulikuwa tunavikagua ambavyo ni vya kuendelea kila siku. Kwa hivyo, siku ile tulipofanya ukaguzi mpaka tulipoandika Ripoti zilikuwa zinafanya kazi kabisa, lakini kwa vile ni vifaa ambavyo vinatumika kila , *breakdown* inatokea wakati wowote.

Kwa hivyo, nataka kumkosoa kwamba hatukufanya kazi kikamilifu; tulifanya kikamilifu lakini unavyojua ni kama kawaida unaponunua gari unaweza kutoka hapo nje ikakataa kunguruma. Kwani wewe hukufanya uamuzi busara? Ni kwa sababu haya ni mambo ya kawaida.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): That is not a Point of Order, you are giving her a lot of information and we are not sure whether she needs your information hon. Member. Okay sit. Hon. Member, please proceed.

Hon. (Ms.) Elina: Mheshimiwa, ningeomba kuzungumza ule ukweli. Tangu mwezi wa tano na wakati Hoja ilipotolewa na mheshimiwa Stanley Kenga, hapa nilisimama nikasema shida ya shilingi 18,000 trekta imelala mpaka sasa. Hata mkiangalia kwenye HANSARD mtapata niliuliza hilo swali siku hiyo. Nikasema kuna trekta ya Magarini hata moja imekuwa ni ya Marafa nimeikuta barabarani inaenda; nilizungumza hivyo hapa Bungeni. Na hivi ninavyokwambia, mheshimiwa, sio kitu kilikuwa kinafanya. Ule mwezi wa tano mpaka sasa ile trekta imelala pale ilipo; haijainuka hata siku moja. Hata hivi ninavyokwambia sasa nimepiga simu na nimeuliza nikaambiwa kwamba bado trekta haijatengenezwa. Kwa hivyo, nataka nikwambie kama Mwenyekiti pia itakuwa ni msaada kwako ili muweze kwenda muangalie shida ilikuwa ni nini na muulize hasa watu wengine kama unaona mimi nakudanganya katika hili Bunge. Nataka kukwambia sijakudanganya; trekta imelala tangu mwezi wa tano mpaka sasa.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Yes, hon. Mbura, a Point of Order or?

Hon. Mbura: I wish to inform the hon. Member.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): He wants to inform you hon. Member?

Hon. (Ms.) Elina: No!

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): She does not wish to be informed. Please proceed.

Hon. (Ms.) Elina: Kwa sababu mimi namwambia kitu ambacho kiko *ground* na itakuwa nimewasaidia. Hata juzi nilikuwa nimepigiwa simu nafikiri na Mbuche alipokuwa anataka Kamati hii ya Kilimo iende Magarini ikaangalie maswala ya unyunyiziaji maji mmea; nikamwambia kunanyesha hatuwezi kwenda mahali pale na hawakuenda. Sasa hii Ripoti wakisema waliikamilisha, waliikamilisha vipi na kwengine hawakuenda? Mungu awabariki. Asante mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Mheshimiwa Karisa.

Hon. Karisa: Asante mheshimiwa Spika. Mimi kwanza wacha niheshimu Kamati ya Kilimo kwa kazi waliyoifanya lakini ningeomba mheshimiwa Spika, sisi waheshimiwa hizi nakala tukipatiwa, tuzisome. Tusipatiwe hizi nakala halafu tukaziacha nyumbani hutuzisomi. Tukawa hutujui Kamati imeona nini kule nyanjani na imepitisha mambo gani pale ambapo yule mtu aliyeliza hilo swali alitarajia nini. Najua wengi hata hapa hawana hizo nakala; wamechukua wameziweka kwenye gari. Swali ambalo liliulizwa na mheshimiwa Stanley Kenga lilikuwa ni; “kwa nini trekta zimelala hasa wakati huu wa msimu wa mvua watu hawalimiwi?” Kamati ya Kilimo ikachukua jukumu nikiwa mmoja wapo tukaweza kuzuru kila gatuzi dogo la Kilifi, na tukapata kwamba ndani ya trekta 53 ambazo tuko nazo katika Gatuzi letu la Kilifi, ni 23 peke

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

yake ndizo zinafanya na katika 30 ambazo zimebaki, 10 zilikuwa zimeegeshwa ni mpya na hata hazijasajiliwa. Ndio tukapata ufafanuzi kwamba katika hizi 30 ambazo ziko pale na zile ambazo zimeharibika, 10 ni mpya kabisa na hazijasajiliwa. Na tulipofatilia, tukagundua kwamba hata yule *supplier* amelipwa; shida aliipata wakati wanasafirisha. Kuna mambo fulani ambayo alikuwa hajakamilisha ndio akawa hawezi kupatiwa zile nambari za usajili wa *tractors* ikabidi tuka *summon* yule *contractor* na hata ukiangalia kila kitu kimewekwa hapa nyuma mheshimiwa Spika. Ukiangalia hata ile kampuni ambayo ilipatiwa ile kandarasi iko hapo hapo lakini hakuna hiyo kama ako nayo ungeweza kuangalia. Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba ndugu zangu kama mlipata hii muweze kusema vizuri; Ripoti hii tukiipitisha kuanzia hii bajeti inayokuja tunaweza kuangalia hii Bajeti inayokuja ndio tutaweza kulima kwa wakati unaofaa kwa sababu utakuta hapa msimu wa mvua *tractor* bado haijatengenezwa; msimu wa mvua *tractor* haina mafuta na hapa tumeangazia kila kitu.

Tumeweka mambo ambayo tunataka ikifika msimu wa mvua kama ni *spare* ziwe ziko katika *store*, kama ni mafuta yawe ya kutosha kusudi tuone ya kwamba zile sehemu ambazo zitakuwa na mvua inaanza mapema *tractors* zinaenda haraka zikalima vizuri kusudi kila mtu ambaye ni mkulima hapa Kilifi aweze kulimiwa vizuri. Sasa hii hujaiona; hapa tunasimama tayari kusema hapana! Someni hii ndugu zangu, mtapata kila kitu kiko hapa. *Recommendations* zote ziko hapa hapa, yale tuliyoona kule tumemuelezea hapa na maofisaa wamefanya jukumu la kuweka hizi Ripoti katika *pigeon holes* na saa hii hakuna hata mmoja ambaye yuko nayo. Siwalaumu kwa sababu hata mimi huchukua hii nakala na naweza kuwa sitaisoma kwa sababu ya shughuli nyingi; nikaweka pale pale lakini ndugu zangu yule ambaye yuko na nakala hii aangalie *findings* na aangalie *recommendations* pale pale.

Zile *recommendations* ambazo ziko pale ndizo zitafanya gatuzi hili la Kilifi na kilimo kiweze kunawiri. Kwa sababu tumepata hata mambo mengine; hatuna mhandisi hapa Kilifi ambaye anaweza kuangalia hizi *tractors* na tumepitisha ya kwamba hapa ikiwezekana katika Ripoti hii tuweze kupata mhandisi kusudi waweze kutembelea hizi *tractors* ziweze kufanya vizuri. Tumepata ya kwamba wafanyakazi wenyewe hawatoshi; utakuta Magarini mfanyakazi ni mmoja na inastahili tuwe na wafanyakazi wa kutosha. Tumepitisha ya kwamba ikiwezekana hata kwa bajeti tuweze kutenga pesa tupate maafisaa wa kutosha kusudi haya mambo ya ukulima tuweke kipau mbele.

Ndugu zangu hamjaangalia hapa; hii Ripoti imepelekwa kwa *pigeon holes* kusudi muone yale ambayo Kamati imeshafanya. Mkisema Kamati haikufanya kazi, je hii nakala mko nayo? Ningewaomba, tukipitisha hii ndio ambayo itatufanya sisi tuweze kulima na mapema, zile *tractors* ambazo ziko kule zimelala ziweze kutengenezwa na mapema, kama ni mambo ya *procurement* yaweze kutengenezwa na mapema, wale maofisaa ambao labda kwa idara yao wanazembea mtaona tumepitisha ya kwamba waweze kuanagaliwa vilivyo kusudi wapate *engineer* atakaye watembelea kwa sababu hakuna wahandisi...

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Yes, summarize hon...

Hon. Karisa: Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba ndugu zangu tuweze kuunga mkono hii Ripoti ili tuweze kulima wakati unaofaa. Asanteni, mungu awabariki.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): The Minority Leader, hon. Matsaki.

The Minority Leader (Hon. Matsaki): Asante sana Bw. Spika. Mimi nimesimama kuunga mkono Ripoti hii. Kusema kweli, Kamati imejaribu kadri ya uwezo wao kuja na Ripoti nzuri ambayo ikipitishwa, haya mambo mengine yanaweza yakapungua katika Kaunti yetu. Kile

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ambacho nataka kuomba haswa kwa Kamati ni kwamba pia ni vizuri kusikize wanakamati wanasema nini kwa sababu ni kupitia kwa wale wanakamati ndio Ripoti hii itapita.

Halafu kitu chengine, tusilaumiane sana hapa hasa wale wanaopinga kwa sababu iko nafasi ya kila mmoja kuzungumza akili yake. Kwa hivyo, hata kama anaongea nini, wewe usimkashifu; wewe usiseme huyu hajui wala huyu hakusoma. Kila mmoja alisoma Ripoti na wakaiona vile ilivyo na ndio sababu mimi pia nimesimama kuunga mkono Ripoti hii ili kwamba kwa mfano Rabai tuko na *tractors* tano; tatu zinafanya kazi na mbili zimelala. Ile Rabai ni kubwa kwa sababu ziko wadi nyengine ni kubwa zaidi. Kwa hivyo, kile kitu ambacho ni muhimu ni kwamba hata zile zimelala hata iwe ni moja pia wale wahusika watakuwa wazitengeneze kwa sababu tayari tumefika katikati hapa but ilikuwa inatakikana kabla kilimo hakijaanza *tractors* zetu ziwe zote zinafanya kazi.

Zile ambazo zimeharibika kama mheshimiwa anavyosema ni sawa; tuseme hiyo pengine ni kutoka mwezi wa tano na Ripoti hii imefanywa baada ya huo mwezi wa tano. Pia itakuwa ni jukumu la kuambiana ili zile nazo ziwe zitatengenezwa na watu wawe watasaidika. Kwa hivyo, mimi ningeomba pia waheshimiwa tupitishie Ripoti hii ili kwamba yale mapungufu ambayo yamepatikana haswa kwa upande wa *Executive* wawe wanaweza wakakaa ngangani na kuhakikisha kwamba kila kitu kitaenda sawa.

La mwisho, kusema kweli Bunge hili la Kilifi tukiwa hapa jamani huenda tukawa kunaweza kuwa na tofauti hapa na pale lakini ukweli ni kwamba nataka niwaambie jukumu letu sisi kama ni *oversight* hatuko hapa kutetea *Executive*; tuko hapa kuona kwamba yale maovu ambayo *Executive* wanafanya tunayagusa na kwamba warekebishe ili huduma za watu wa Kilifi ziwe zitaweza kupatikana kikamilifu. Kwa hivyo, ninaomba nikae lakini naunga mkono Ripoti hii. Asanteni.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): The Member for Kibarani but before that I want to inform Members one thing; that we cannot blame the Executive so far because we have not taken this Report to them, so unless we have adopted the Report today then it will be taken to the Executive. I think that is clear as we make our contributions. The Member for Kibarani.

Hon. Mwamutsi: Mr. Speaker, I appreciate you for giving me this opportunity also to give my contribution. I think this House is represented by the Committees to dig into the deep aspects of the various challenges that we have as a people. The Committee for Agriculture was mandated by this House to go dig deep in matters of how these tractors were supposed to be used. I have full faith in the Members of the Agriculture Committee, so the Report that we are discussing today I think is made to make this Department perform much better than how it was performing before. So, the challenges that my colleagues are speaking about I think is part of the problem that this Report is supposed to solve. As I support this Report, Mr. Speaker, we also need to give some input to prove it.

As shown by the Report here, we have about 23 tractors in the county but their usage has been in question. Like the table here that shows the amount of money that these tractors have been bringing to the county, this amount is too low. The amount of money spent on these tractors and the amount of money spent on repairing these tractors is not equivalent to the amount of money that the tractors are bringing into the county. I think that is because of the mechanisms those that are charging money are using.

I support this Report. I appeal to the Agriculture Committee to put more effort in ensuring that as people are hiring these tractors, money is not lost because you cannot say that the whole of the agricultural period, it is only 22 acres that were ploughed in Kibarani Ward.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

This is a Joke! 22 acres Mr. Speaker! If we can put it that we need to be food sufficient, 22 acres cannot feed the people of Kibarani. If I can take Kibarani as an example, there is much to be done. Thank you. I support this Report although we need to ensure that it is more effective. Thank you, Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Yes, hon. Alphonse Thuva

Hon. Pascal: Asante Mheshimiwa Spika, japo jina langu si Alphonse naitwa Pascal Thuva. Nachukua nafasi hii kuunga mkono na kuwapongeza wanakamati ambao wameleta Ripoti hii katika Bunge hili la heshima. Tumekuwa na azimio la kulenga kuleta chakula bora na cha kutosha katika Kaunti ya Kilifi. Na ndani ya kutimiza haya tumejua mwanzoni kwamba kumekuwa na shida ndio maana tukapeana wajibu huo kwa Kamati ambayo tunaiheshimu na iliweza kutuletea ni shida gani ambayo inakumba sekta hii. Shida ni matingatinga kutoweza kutimiza wajibu wake.

Katika Ripoti hii, tumeweza kuelezwa kwa undani shida ambazo zimesababisha *tractors* hizi haziwezi kufanya kazi. Katika mambo haya ambayo yameelezwa hapa, moja wapo ni ukosefu wa wafanyikazi wa kutosha, kukosa mafuta ya *tractor* na shida nyingine nyingi zimeweza kuelezwa hapa na labda ni jukumu sasa la sisi ambao tumepewa Ripoti hii tujue ya kwamba tutafanya nini ili tutatue shida hizi na *tractors* hizi ziweze kufanya kazi.

Kuna hiyo shida ambayo mheshimiwa wa Kibarani ameangazia saa hii ya kuwa *tractors* hizi haziwezi kuwa zimelima ekari 20 peke yake katika Kibarani. Na mbali na Kibarani tunazo wadi nyingi ambazo vile vile zilikuwa zinalenga kufanyiwa kazi na *tractors* hizi. Lakini shida ambazo zimeangaziwa tunaona ukosefu wa mafuta ni jukumu kama tumenunua *tractors* hizi, tuone ni vipi zitakuwa zikihudumiwa nazo. Kwa sababu *tractor* kawaida inahitaji mafuta na wafanyikazi ndio iweze kuleta yale mazao ambayo tunatarajia kama Kaunti.

Sasa tumeona zile shida ambazo zimeangaziwa hapa. Tunalo jukumu la kuzishughulikia haraka iwezekanavyo ili msimu wa kilimo ukifika tuwe tumeweza kutatua hizi shida. Vile vile, tumeona mapato ni machache lakini tuna haja ya kufikiria je, *tractors* hizi tunazikodisha kwa pesa ngapi ili mkulima aweze kulipa? Kama sikosei, bei iliyowekwa ni shilingi 1,000 ama shilingi 1,500. Na jinsi zinavyofanya kazi, je mapato yale yana uwezo wa kurekebisha zile *tractors* kama pengine ziko na shida na je, kuna uwezo wa kupata mafuta kwa wakati unaofaa?

Ni lazima tuangalie mapato na vile tunavyohudumia hizi *tractors* zetu kama Kaunti. Kwa hivyo, tuna jukumu vile vile la kupiga darubini na tuone kwamba tunawekea ama tuna *service tractors* hizi vile inavyohitajika. Kwa sababu hatuwezi kuwa tunahitaji zitupatie mapato makubwa halafu katika kuzitunza tuwe tunazinyima vitu fulani. Na nikimalizia, mheshimiwa Spika, naomba waheshimiwa tukiwa hapa sisemi ati tufunge midomo lakini vile vile tuna haja ya kupata mwelekeo kwa wale wanakamati. Mara nyingi tumeona labda kuna *Point of Information* wengi wetu tumekuwa tukikataa lakini pata mwelekeo kutoka kwa wale wanakamati. Lakini ni vizuri pia kama mtu amekosa ufahamu aweze kumpa mheshimiwa mwenzake nafasi ya kuelezwa ili tuweze kuwa katika muongozo mzuri wa kufahamu jambo fulani. Asante mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono Ripoti hii.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): That was a very good contribution from hon. Pascal Thuva. I am sorry I introduced you as Alphonse but there is no problem you are both seniors so I respect you. The Member for Gongoni, please, then we go to hon. Changawa.

Hon. Kiraga: Thank you so much Mr. Speaker, Sir. If there is a Department which has failed this County is the Department of Agriculture. Agriculture is one of the big four in the country and one of the big five in the county. But the deeds of the Department do not marry the

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

happenings. You have heard some Members talking very aggressively against this Report. First and foremost, I was against this Report just because I had not read whatever that was in this Report but thanks to the hon. Member for Bamba (Hon. Mwambire) who has tried to share a copy with me.

Let me first of all congratulate the Committee for the job well done, led by hon. Noordin, the Member for Kaloleni and the other Members. If you look at the findings in this Report, they are not different from the concerns from the Members who have contributed. It now tells us that this Committee had the heart of the Assembly and the people of Kilifi and if you go through these findings you will see all these concerns. They have also noted that tractors were procured and kept in a yard for almost one year. That is one of the findings. They have also noted that the charges for ploughing our farms were Kshs1,500 contrary to the Finance Act which we passed...

(Hon. Kiraga spoke off record)

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Do we have another microphone?

Hon. Kiraga: Okay thank you so much Mr. Speaker. They have been charging Kshs1,500 contrary to the approved charges which are also captured in the Finance Act, 2018. They have also talked of fueling, which has been a very big problem to the tractors. They have even talked of the inability of some of the drivers to operate these machines. It is in the Committee findings. On the ground, you will see a form four leaver but some of those guys cannot operate those tractors. If you look at the recommendations of the Committee, they marry the findings and I believe if we approve this Report and the Executive implement whatever is here, then I think as a Department and as a county we shall be moving in the right path.

Mr. Speaker, I know the Department is faced with a lot of challenges. It has failed this county. It has been having some very substandard projects. If you look at the budget since the financial year 2013/2014, you will see all wards issues and that has not helped this county and that is why during the budget making process, we collapsed all issues concerning all wards. We would wish the Sectoral Committee that is Agriculture Committee, to put this Department on its toes because without that, this county will not move.

We are not comfortable to budget for relief food, to put Kshs200 million for relief food; that is a waste. Why don't we use this Kshs200 million to do a mega project which will alleviate these problems in this county? Mr. Speaker, as I windup, I really thank the Committee and as I have noted earlier here that at first I was very much against the whole issue but looking at this Report, the Committee has done a commendable job. Thank you.

(Applause)

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Yes hon. Changawa.

Hon. Changawa: Asante mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii kuchangia mada ambayo iko mbele za Bunge hili juu ya utenda kazi wa *tractors* na Ripoti hii ya Kilimo. Nimesimama kwanza kueleweka kwamba ninaunga mkono *100 percent* Ripoti ya Kamati hii na kueleza tu machache nikiungana mkono na mheshimiwa *Sonko* (Karisa); ni *Sonko* kwa lile jina la mtaa ya kwamba aliyoyanena yalikuwa ya kweli na ya muhimu.

Kwangu nataka tu niseme ya kwamba kuna utofauti ya *Statement* ama swali limeulizwa kwa waziri wa idara na kujibu, na waziri huyu amejibu visivyo. Lakini Kamati imepewa jukumu

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

la kurudi tena chini ili kutafuta ukweli wa swali lililoulizwa. Haya ambayo yako hapa ni yale ambayo mheshimiwa Stanley (Kenga) aliyauliza ili kuhakikisha kutakuwa na mabadiliko katika sehemu ama wizara hii ya Kilimo na Kamati imechukua nafasi hiyo ili kuona katika ule uchache waziri alijibu basi Kamati inakuja kujibu hili swala lote kwa upana.

Nasema *we shall call a spade a spade; Executive* imetufeli kwa mda mrefu na hatutakubaliana na mambo ambayo yatakuwa yanaenda visivyo. Kila mmoja mpaka yule ambaye hajasoma, yule mama Kadzo kule mashinani, anajua kabisa msimu wa mvua na wa kupanda ni gani. Kama wizara itaenda kutayarisha mwezi wa sita ama wa tano yale ambayo yanahitajika yaweko kabla ya Januari ama mwezi wa pili mvua ikianza ndio tutalalamika na njaa kwa sababu ya watu wanaokosa kuwajibika. Mswada huu nikiangalia yale mapendekezo ambayo Kamati imeweka inaonyesha kwamba kuna mahali kuna makosa.

Tukiangalia nambari ya kwanza, nitasoma tu kwa Kiingereza vile imeandikwa; *“That by the end of May 2018 all the grounded tractors should be operational. The Directorate should ensure that spare parts are available and repairs are done immediately.”*

Tukiangalia mapendekezo nambari ya pili inasema, *“That by 25th May, 2018, the ten new tractors should be operational with logbooks and number plates.”*

Mheshimiwa Spika, kama tuko mwezi wa saba na Kamati imekaa na kupendekeza mambo haya yafike kwa Wizara ili marekebisho yafanywe, kama tutapitisha leo ikifika tuko mwezi wa ngapi, tayari tutakuwa tumefeli ama kuchangia kufeli kwa hiyo kamati.

Kwa hivyo, tunasema hata kama Bunge litakuwa na shughuli nyingi lakini pia yale ambayo yanataka kushughulikiwa mapema ili kusaidia hali za wakulima wetu yaletwe Bungeni mapema ili marekebisho yafanywe. Hata kama ni kikao cha dharura lazima tuje ili tuhakikishe ya kwamba haya mambo yanapitishwa maana kama Kamati imeweka mwezi wa tano na saa hizi ndio itaenda kule kwa *Executive*. Kupitia kwa yale maneno yako mheshimiwa Spika ambayo umesema...

(Hon Kambi stood on a Point Of Information.)

The Temporary Speaker (Hon.Thaura): What is wrong hon. Kambi?

Hon. Kambi: Naomba kumfahamisha kitu kidogo.

Hon. Changawa: Sitaki kufahamishwa tafadhali.

The Temporary Speaker (Hon.Thaura): But I also think it is good because I have discovered there is something that the Committee knows that we do not know as a House, unless you really do not want to be informed.

Hon. Changawa: Kwa heshima yako mheshimiwa Spika, niko sawa kabisa kama atanipa taarifa pengine nje baadaye.

The Temporary Speaker (Hon.Thaura): Okay, mheshimiwa Renson (Kambi) please put your point before we conclude.

Hon. Karisa: Mheshimiwa Spika, ndugu yangu mpendwa ninayekupenda, hii Ripoti nafikiria ni mara ya tatu wakati tukiileta hapa, yule aliyeleta hii Ripoti hakuwako. Na kulingana na hiyo tarehe, Kamati iliweza kufuatilia mpaka saa hii hizo *tractors* kumi ziko na nambari za usajili zote. *Spare parts* ya zile *tractors* 30 ziliingia. Na zile zilizoharibika tayari *spare parts* ziko hapo. Tungeomba hii ingerudishwa wakati unaofaa saa hii zile zingine zingekuwa zinafanya kazi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kwa hivyo, ningepomba tu kuongezea kwamba nambari za usajili za *tractors* 10 ziko tayari na Ripoti ingekuwa imepitishwa mapema watu wengine wangelimiwa msimu huu.

The Temporary Speaker (Hon.Thaura): Okay, wind up hon. Changawa.

Hon. Changawa: Asante mheshimiwa Spika lakini nafikiria hayuko mbali na mimi. Ilikuwa ni kupitia yale maneno yako ambayo umeyasema kwamba tupitishie iende kule ndio iwe *adopted*. Kwa hivyo, kama yamefanywa yatakuwa yamefanywa kabla ya kupitishwa.

Kazi nzuri imefanywa na Kamati ya Kilimo. Cha msingi tuiptishie ili yasifanyike tena yale ya kucheleweshwa kwa *tractors*. Na nilikuja nikasema *tractor* ...

The Temporary Speaker (Hon.Thaura): Please wind up.

Hon. Changawa: *Tractor* haipalilii. Asante mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon.Thaura): The Chairperson for the Committee and you will be winding up the contributions.

(Question, that the mover be now called upon to reply, put and agreed to)

Hon. Noordin: Asante mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono Mada hii. Nataka kuwaambia waheshimiwa wenzangu kwamba tulipoingia kwa Kamati hii, yale tuliyoyaona kule nyanjani yalikuwa ni ya kusikitisha sana. Hayo ndio yalitufanya tuweze kuingia ndani kabisa kuweza kujua vitu vingi ambavyo waheshimiwa wengi labda hawavijui.

Kuna mambo mengi ambayo tuliyakuta hayako sawa. Kusema idara haiko sawa ni kweli haiko sawa kwa sababu wengi huwa hawafanyi kazi ambayo wameajiriwa nayo lakini mengi huwa yanaturegelea sisi hapa Bunge. Kwa hivyo, yale ambayo tuliyakuta kule ni yale ambayo tulifanya mapendekezo na ndio ambayo tuliandika katika karatasi hii na tukaileta hapa Bungeni; ndio ile mlikuwa mmeekewa kwenye *pigeon holes*. Kama kweli hukupitia labda ni kwa sababu ya shughuli nyingi lakini kama ulipitia utaona kwamba kuna maswala ambayo tulienda ndani kabisa ili tupate kujua ni kwa nini madereva wanaiba wakienda mashambani. Tukapata kujua ni kwa sababu mtu kama dereva yuapewa *tractor* na hapewi na chakula wala nini. Asubuhi anaenda nalo shamba mpaka jioni. Huyu ni binadamu atakula nini? Kwa hivyo lazima afanye nini? Afanye mchezo. Kwa hivyo, tulipata sehemu nyingi ambazo kuna *loopholes* ambazo watu walikuwa wanakula pesa. Hizo zote tuliweka kwenye mapendekezo na Mungu akipenda ni kwamba tunapopitisha swala hili basi itakuwa tumeanza ama tumeingia kwenye mwamko mpya.

Lengine ambalo nataka kusema ni kwamba sisi wenyewe kama waheshimiwa tujiulize katika bajeti zetu ni watu wangapi wameweka hili swala ambalo tunaliita kipao mbele, tunaliita kwa mdomo lakini ni tuangalie ni watu wangapi ama waheshimiwa wangapi wamechukua pesa zao za kwenye wadi na kuweza kusaidia kiupande wa ukulima. Tutapata hakuna. Kila mmoja anakimbilia upande wa majengo ya elimu na wengine wanakimbilia mambo ya maji. Ni tusimamame wima kuonyesha kwamba tunaweza kuondoa ama kueneza hili swala la kusema kwamba tunataka kutupilia mbali njaa.

Kama hatutaweza, sisi wenyewe pia kama waheshimiwa kwenye *docket* hii kuweza kuweka chochote kwa upande wa ukulima, basi nafikiria tutakuwa na shida sana. Nimesimama kuunga mkono na ninataka kuwaomba waheshimiwa wenzangu tupitishie hii kwa sababu tukipitisha tu, Mungu akipenda yatakuwa na mafanikio mazuri. Asanteni.

The Temporary Speaker (Hon. Thaura): Hon. Members, having contributed fully and listened to the contributions of your fellow Members, I am sure you now have a resolution whether to support or deny this Report. So I will now put the Question.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Question put and agreed to)

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

AVAILABILITY OF SPORTS EQUIPMENTS

I have a Communication that the sports equipment have already arrived and are within this building. All Members are requested to be available for practice at Malindi High School as early as from today. From this sitting, kindly proceed to Malindi High School for engagement in the different sports that will be available. For one to be allowed to attend the tournaments outside the county, you will need to avail yourself from today. So, all Members and particularly my friend hon. Shaban, you are requested to join the team immediately.

ADJOURNMENT

There being no other business, this House stands adjourned until tomorrow at 2:30 p.m.

The House rose at 3.24 p.m.